THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/2

# KISWAHILI 2

*(Kwa Watahiniwa Walioko na Wasiokuwa Shuleni)*

*Muda : Saa 3* *2009 Februari, 13 Ijumaa, Asubuhi.*

---

*MAELEKEZO*

1. Karatasi hii ina maswali **14** katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **Matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Maswali **yote** yana alama sawa.
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 6 zenye maandishi.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

## FASIHI KWA JUMLA

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

1. (a) Eleza vipengele muhimu vya fani na maudhui vijengavyo kazi ya fasihi andishi.

   (b) Eleza uhusiano uliopo kati ya fani na maudhui.

2. Chagua tanzu mbili za fasihi kisha onesha zinavyotofautiana.

3. "Utamu wa uwasilishaji wa kazi ya fasihi andishi hutokana na mchango mkubwa kutoka katika fasihi simulizi". Thibitisha ukweli wa kauli hii.

## SEHEMU B (alama 20)

## USHAIRI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

| | | |
|---|---|---|
| **Kimbunga** | - | **H. Gora** |
| **Mapenzi Bora** | - | **S. Robert** |
| **Chungu Tamu** | - | **T.A. Mvungi** |
| **Wasakatonge** | - | **M.S. Khatib** |

4. Chagua taswira **nne (4)** kutoka katika vitabu **viwili (2)** ulivyosoma, kisha jadili jinsi waandishi walivyozitumia taswira hizo kama mbinu ya kufikisha ujumbe kwa jamii.

5. "Washairi wanatamba katika mawanda mapana ndani ya jamii, wakiadibu na kuburudisha bila hofu yoyote". Thibitisha kauli hiyo ukitumia vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

6. "Msanii bora ni yule anayeisaidia jamii yake kupata mwelekeo chanya wa maisha". Jadili tamko hili ukilihusisha na vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

## SEHEMU C (alama 20)

## RIWAYA

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

| | | |
|---|---|---|
| **Janga Sugu la Wazawa** | - | **Gabriel Ruhumbika** |
| **Barua Ndefu Kama Hii** | - | **Mariam Ba** |
| **Pesa Zako Zinanuka** | - | **Ben R. Mtobwa** |
| **Vuta N'kuvute** | - | **Shafi Adam Shafi** |


Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

7. "Jamii ndiyo inayomfinyanga msanii, hata akakomaa na kuweza kutoa zao la kazi ya fasihi kutokana na mazingira ya jamii hiyo". Jadili kauli hii ukitumia vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

8. Tathimini mitafaruku iliyojitokeza katika vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

9. Waandishi huwahusisha wahusika wa jinsi zote kwa madhumuni ya kupambanua na kuweka wazi matatizo yanayoibuka katika jamii. Eleza mahusiano hayo kama yanavyooneshwa katika vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

## SEHEMU D (alama 20)

## TAMTHILIYA

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

| | | |
|---|---|---|
| **Kwenye Ukingo wa Thim** | - | **E. Hussein** |
| **Morani** | - | **E. Mbogo** |
| **Kivuli Kinaishi** | - | **Said Mohamed** |
| **Nguzo Mama** | - | **P. Mhando** |

10. Onesha mikakati **minne (4)** inayotarajiwa katika kuleta mafanikio chanya kama inavyojadiliwa katika vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

11. Kwa kutumia vitabu **viwili (2)** ulivyosoma jadili jinsi mitindo ilivyopevusha ujumbe uliomo.

12. "Tamthiliya isipoumbiwa mandhari imara, inakosa uzito katika kusawiri hali halisi ya jamii". Jadili mandhari katika vitabu **viwili (2)** ulivyosoma.

## SEHEMU E (alama 20)

## USANIFU WA MAANDISHI

Jibu swali **moja (1)** kutoka sehemu hii.

13. Soma shairi lifuatalo kisha jibu maswali yanayofuata.

Niliota kwa yakini, niliota ndoto tatu,
Nalala usingizini, niliota mara tatu,
Ni kweli nawambieni, niliota siku tatu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Maana yake ni nini, ya kuota ndoto tatu,
Mwezaye **kubaini**, anieleze kiutu,
Na niliota kwa nini, mfululizo siku tatu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Nilipita darajani, njia ipitayo watu,



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Hilo daraja kwa ndani, lina maji **metu metu**,
Na humo ndani majini, mna mzoga wa chatu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Pili niliota baharini, mfano bahari yetu,
Zi samaki baharini, zaidi ya laki tatu,
Zina vichwa mkiani, si mfano wa za kwetu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Tena zina vichwa vya kichwani, mfano wa za kwetu,
Kichwani na mkiani, vichwa viwili viwili ni "kitu",
Ni kitu kweli yakini; kushangaza vichwa vyetu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Tatu naota nyumbani, nilikozaliwa kwetu,
Naota nyumba zamani, ya **raham** baba yetu,
Yaongezwa kwa hisani, juu kwa tofali tatu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Nimesahau baini, ndoto ya pili si tatu,
Kwa ndoto ya baharini, nimemsahau mtu,
Alipita baharini, kwa baiskeli si yetu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Anapopita majanini, ajabu yake mwenzetu,
Nyuma yake mgongoni, kunakauka **kukutu**,
Wanachuoni nipeni, ajabu ya ndoto tatu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

Hili sifumbo katani, ninaapa baratu,
Siku moja na yakini, huziota ndoto tatu,
Na ndoto hizo amini, nimeota siku tatu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

**Kaditama** kitabuni, jibuni mambo kwa utu,
Mwakipita Selemani, pokea gari ni vitu,
Ijapo pindi mwakani, tutaonana si kitu,
Niliota ndoto tatu, maana yake ni nini?

**MASWALI**

(a) Nini maana ya maneno yafuatayo:-

(i) Kubaini.
(ii) Metumetu.
(iii) Raham.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

(iv) Kukutu.
(v) Kaditama.

(b) Eleza maana ya taswira zifuatazo:

(i) Bahari.
(ii) Samaki.
(iii) Baiskeli.
(iv) Mzoga wa chatu.

(c) Andika kichwa cha shairi kisichozidi maneno **matatu (3)**.

(d) Eleza umbo la samaki aliowaona mwandishi. Umbo hilo linaashiria nini?

(e) Shairi hili kwa jumla linaweza kuwa linazungumzia nini?

(f) Katika ubeti wa **nne** kuna makosa ya matumizi ya lugha. Bainisha makosa hayo na uandike ubeti huo kwa usahihi.

14. Soma habari ifuatayo kisha eleza mbinu za kifani zilizotumiwa na Msanii ili kufanikisha kazi yake.

Basi bwana tukafika sehemu ikabidi Tolu ashuke na mimi niendelee na safari. Bwana na hapo ndipo kasheshe ilipoanza mwanangu.

Kumbe yule dada alitaka sana kuongea na sisi bali alikuwa akimuogopa Tolu. Pale Tolu aliposhuka tu, akaona huo ulikuwa ndio wakati muafaka wa kunichombeza kwa hiyo kuanzia hapo ndio tukaingia katika chombeza taim.

Unajua aliningia na magia gani? Aliniuliza eti lile jirafiki lako mbona jirefu vile? Mh! Mimi nikaona yule dada alikuwa anataka kuniletea gozigozi tu, yaani ametoka huko amejikusanya na mikorogo yake yote ili kuniuliza swali hilo tu, haya, nikamjibu kuwa yale ni maumbile tu ya mtu kwa hiyo hilo lisimsumbue kichwa.

Hakuishia hapo, dada huyo ambaye kumbe nilikuwa nimemtazama kwa woga hapo mwanzo, sasa baada ya kumsogelea kwa karibu nikagundua kuwa alikuwa ni mama mzima, Looh! Nikaanza kuogopa kwa maana nimesikia stori kuwa kuna wakina mama watu wazima wanatabia mbaya ya kuwapenda watoto wadogo kwa sababu eti damu yao bado ina boili! Bho! Nikaona hataa, leo lazima niuone mwisho wa huyu mama maana anaweza naye akawa mmoja wa hao mashuga mami ambao tabia zao ni kuwarubuni vijana wa kiume na kuwachezesha gwaride la utambulisho bila hiari yao.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

Basi bwana yule mama akaendelea kuniandama na maswali akiniuliza eti ninakaa wapi? Nikamjibu ninaishi na sisita wangu huko Ukonga na mara nyingi huwa niko na braza wangu hapo chovenye wa coca cola ambaye anaishi Sinza.

Akaniuliza eti mimi ni meredi au bachela? – Eh! Alipofika hapo sasa nikaanza kuelewa kuwa hili ndilo lenyewe shuga mami, kwa nini linaniuliza maswali ya ndani kama haya?

Hapo nikaanza kubadilika kidogo usoni na kujifanya siko soo interestedi na maswali yake na sio kwamba nilikuwa napenda kudili naye - - Noo! Nilikuwa kazini kupata ukweli kuwa ni kweli atataka kuwa klozi na mimi au la ---.

Sasa akawa kama anataka kuniambia kitu lakini akawa anachachawa kiaina tu, basi nikamuanza mimi kwa kumuliza kwani ulikuwa unasemaje? Mbona unaniuliza maswali kama hayo? Akaniambia kuwa amevutiwa sana na pesonalite yangu na kwa hiyo angefurahi sana kama angekuwa na karilesheni kakaribu na mimi. Unaambiwa miguu yote ikaanza kuninyong'onyea kwa woga, hivi ni kweli mama ndio ananiangushia machunusi jamani mbona kazi!! – Ama kweli chunusi sio baharini tu, hata kwenye madaladala wapo!

Huyu alikuwa mama wa makamo aliyeshiba vilivyo. Mguu alipata, ndombolo ndio usiseme manake huko kwa kigoda ndio kulikuwa kunaashiria kuwa kazi kwenu, na ukija huko kwenye nido zilikuwa wala hazitishi sana. Alikuwa anavutia kwa kweli na kama wangekuwepo wale wataalamu wa mambo ya nani huyu wangempitisha kuwa Miss Mashuga mami.

Lakini ndugu yangu msomaji huko usoni yule mama alikuwa amekoleza mkorogo ile mbaya yake. Mimi mwenyewe ati festi nilijua yule mama alikuwa mtashe fulani aliyeshuka juzi kutoka Mamtoni, nilishituka sana pale aliponisemesha kibongo.

Ah! Lakini mwisho wa yote bwana, ni pale aliponiomba niende naye nyumbani kwake ndipo nilipoamua kumuliza hivi wewe mama una mume? Akaniambia yeye sio meredi ila ana kabuzi kake ambako kwa wakati huu kako safarini na mvua ndio kama hivyo tena, kwa hiyo angefurahi sana kama ningekaimu nafasi ya hako kabuzi kake!! --.

Nikamwambia kwa sasa niache niende nyumbani nikaoge, lakini nikamuliza nimkute wapi? Akaniambia nimfuate Sheraton na pesa ya teksi akanipa ili nisiikose promisi yake.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org